MWITO PROG 1092 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 5:19

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1092 kutoka studio zetu za Nairobi.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini mkubwa wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake Harod Williams.

Na ikiwa msikilizaji hukuwa nami kwenye makala yaliopita ningependa kukuarifu kuwa tulisoma aya ya 17 ya Warumi 5….… ***kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti yalitawala kwa sabbu ya yule mmoja,zaidi sana wao waokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki watatawala katika uzima kwa yule mmoja,Yesu kristo.***Hebu tuendelee na aya ya 18**……*Basi tena kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu,kadhalika kwa tendo moja la haki,watu wote walihesabiwa haki yenye uzima.Kwasababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi,kadhalika kwa kutii kwake mmoja,wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki*.....**naomba niongezee aya ya 19 kwa kuwa ndiyo msingi wa somo la leo…. ***kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi,kadhalika kwa kutii wengi wetu wameingizwa katika hali ya wenye hak***i.Aya ya 20……**Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana,na dhambi ilipozidi neema ilikuwa nyingi zaidi.Aya ya 21….ili kwamba kama vile dhambi iliyotawala katika mauti,vivyo kwa**

**njia ya haki neema itawale hata uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu.**

Mpendwa tunaendelea na somo letu ,ambapo tunakaribia kumaliza aya ya 5.Na kwa sasa ningependa niseme somo hili limekuwa la kuridhisha na la kufahamisha mengi.Sijui wewe lakini kwangu mimi limkuwa la kunifaa sana.unapochunguza aya kwa aya takuta kwamba umepata ufahamu wa sehemu nyingi muhimu za bibilia na hatimaye bibilia nzima.Hutakuwa na mtindo wa kuchagua tu sehemu za Bibilia unazozienda na kuzikariri.Ikiwa tutapenda na kuchagua tu sehemu za bibilia tunazozifahamu na ambazo ni muhimu tuzisome na kuzielewa.Ukweli kwamba haikukufaa wala kuendana nay ale tunayotaka,haimaanishi si nzuri kwetu.Kuna sehemu muhimu ambazo zinatuasa na kutuonya ili turekebisho mienendo yetu.Nyingine hazitakuwa nzuri kwetu.Ukweli ni kwamba tutatoa hesabu ya kila tulilotenda hapa duniani.Baadhi yetu kuna maandiko tunayapita tu kwa kuwa hayatupendezi.Tunona hayatufai,lakini hilo ni neno la Mungu.Na kwalo utahukumiwa.Najua hapo nyuma tumepitia maneno ambayo si ya kawaida.Kanuni za kidini na maneno ya kifalsafa na kithiolojia.Madhumuni ya mafundisho haya ni kuchambua aya kwa aya,sura kwa sura ya kuyafafanua na kuyarahisisha maeno hayo ili tupate kuangaziwa ukweli.Tumepitia maneno kama vile kuhesabiwa haki na kuwajibikia msalaba.Lakini katika yote ukweli ni kwamba Mungu kupitia mwanawe Yesu Kristo alikinunua kizazi cha binadamu kilichokuwa kiovu.Kumbuka tangu sura ya kwanza ya kitabu hiki cha Warumi kuna watu walitenda dhambi .Walimkosea Mungu.Walikuwa na hatiambele za Mungu.Watu wa mataifa walikuwa wametenda dhambi ,jinxi wayahudi pi walitenda dhambi.Mungu aliwaona wote waovu.Walikuwa wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Jinsi tulivyosoma kwenye aya ya 18…. ***Basi tena kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu,kadhalika kwa tendo moja la haki,watu wote***

***walihesabiwa haki yenye uzima.***Na vivyo hivyo katika ukurasa wa 18 kupitia mtu mmoja yaani Adamu wa pili ambaye ni Yesu Kristo kwa mujibu wa somo letu,alikuja kuokoa kizazi hiki.Hata hivyo kuna jambo ningependa kusema hapa.Sote tulitenda dhambi kwa ajili ya kuwa warithi wa dhambi ya asili ya Adamu.Lakini kuhesabiwa haki na wokovu kutokana na Yesu,si kwa kila mmoja.Hapana wokovu wa jumla.Ni kwa wale watakaotubu dhambi zao na kuokolewa ndio watauona ufalme wa Mungu.Tokea Mwanzo hadi Ufunuo hakuna wokovu wa jumla.Ni dhahiri kwamba wengi wataangamia.Njia ya kwanza ni kwenda mbinguni ,nayo ya pili ni kuonana na Yesu nayo ya tatu,wimbo ulisema hupita wachache watu wengi wataangamia.Wachache watapita njia ya wokovu.Njia ile nyembamba inayowajibiha waja kwa Kristo kupitia wokovu.

Mpendwa Yesu anakupenda na anataka uokoke.Hata hivhyo hutaazimihwa wokovu.Ni kwa hiari yako.Waweza kuahirisha na kuufanya moyo wako kuwa mgumu kama jiwe.Hiyo ni shauri yako,lakini mwishowe ukifa kabla ya kuokoka utakumbana na hukumu.Ama utaishi na muumba wako milele au utaihia Jehenamu palipo na vilio na kusaga meno.Mauti ya milelde.Kumbuk Bibilia inasema kwamba …kadiri ya wale waliomjia Yeye Yesu Kristo na kumpokea aliwafanya wana,lakini ambao hawakumpokea walihukumiwa kifo cha milele huko Jehenamu.

Tumalizie na aya ya 20 ya Warumi 5…..…. ***Basi tena kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu,kadhalika kwa tendo moja la haki,watu wote walihesabiwa haki yenye uzima***. Aya ya 20.... ***Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana,na dhambi ilipozidi neema ilikuwa nyingi zaidi.***

Rafiki hangu MUngu alituachia neema nyingi tu.Tulikumbushwa katika aya ya 17 kwamba… ***kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti yalitawala kwa***

***sabbu ya yule mmoja,zaidi sana wao waokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki watatawala katika uzima kwa yule mmoja,Yesu kristo.***

Kwenye sura ya 4 tuliambiwa kuwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa mujibu wa imani yake.Nasi pia wale tuliomwamini na tuna imani kama hiyo na kupitia neema ya Kristo Yesu tulihesabiwa haki.Naomba kabla ya kutamatisha somo hilo nitoe mwaliko wa wokovu.Chukua fursa hii utubu hambi zako na urekebishe uhusiano na Mungu muumba wako. Una hakika utamwona Kristo atakapordi kuwachukua walio wake? Wale ambao wameokoka na wanafanya kazi yake? Fursa ni hii ikiwa hujamjua Kristo kuwa mwokozi wako.Tubu dhambi zako sasa n umwendee ndugu u dada aliyeokoka na ushiriki naye kuhusu uamuzi uliofanya.Aidha mwendee mchungaji wa kanisa linalohubiri wokovu wa Yesu Kristo.Atakushauri na kukuelekeza jinsi ya kukuza imani yako. ? nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi Utamfungulia mlango wa moyo wako ili apate kuingia?Ikiwa jibu lako ni ndio ningependa utubu dhambi zako leo na kumpokea rohoni mwako ili akue dira mpya maishani mwako.Usije ukatahayari siku ya mwisho,wakati wateule wake watakapopanga foleni kuingia Jerusalemu mpya.Mbinguni ambako tumeandaliwa makao.Chukua hatua hiyo sasa hivi.Ninasubiri uchukue hatua hiyo ,kisha uniandikie au unitumie ujumbe mfupi.Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1092 Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia

kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 19 ya sura ya pili ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.Kwaheri.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx